




Food and Agriculture Organization of the United Nations



USAID
KUTOKA KWA WATU
WA MAREKANI



UGANI KIGANJANI DARAJA LA MAENDELEO YA KILIMO



Hali Ya Hewa Na Mazao

Mifugo Na Uvuvi

Taarifa Za Soko Na Bidhaa

Uhifadhi Virutubishi Na Ubora

M-Kilimo

Huduma za ugani kilimo mkononi mwako

Kuelekea mapinduzi ya kidigitali katika kilimo kwa huduma bora, jumuishi na zinazoendana na mabadiliko ya tabianchi bila kumuacha mtu nyuma.



© FAO/Ami Vitale

UGANI KIGANJANI

- Mfumo wa kibunifu, rahisi na wa gharama nafuu unaotumia mtandao kupeleka taarifa na huduma za ugani kilimo, utabiri wa hali ya hewa na ushauri, kalenda ya mazao, uhifadhi virutubishi na lishe, mifugo na uvuvi nchini Tanzania.
- Unatoa taarifa za kipekee na uhakika zinazohusu sekta ya kilimo na zinazotolewa na wizara na taasisi husika nchini Tanzania.
- Ni sehemu ya huduma za kimtandao zinazotolewa na shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) kwa wanachama wake.
- Huduma hii inatolewa kwa kusaidiana na huduma nyingine za kidigitali kwenye kilimo nchini Tanzania ikiwamo M-Kilimo na EMA-i.
- Inatoa majibu ya uhakika kwa wadau wote wa kilimo, chakula na lishe kwa ngazi mbali mbali kutokea kwa mkulima mdogo hadi serikali kuu.

HUDUMA KWA YEYOTE, WAKATI WOWOTE, POPOTE

Njia ya kuelekea kilimo kipya

- Yeyote ambae anavutiwa na sekta ya kilimo na wenye lengo la kufanya mabadiliko ya hali ya maisha kwa kupitia njia bora za kilimo endelevu na kutunza mazingira.
- Ikiwalenga wavuvi, wakulima wa mazao, wafugaji, madaktari wa mifugo, wazalishaji chakula cha mifugo, wafanyabiashara, wauza pembejeo, wazalishaji mbegu, watafiti, maafisa ugani, wafanya maamuzi na watunga sera.

Ufahamu umeletwa karibu zaidi

- Wakati wowote, katika kuboresha uzalishaji na urahisi wa kufanya maamuzi sahihi katika sekta ya kilimo, mifugo na uvuvi.
- Wakati wa kufanya maandalizi ya shamba, kupanda, kupalilia na kuvuna kwa kutumia taarifa sahihi na za wakati kulingana na eneo husika.
- Wakati unapohitaji taarifa sahihi juu ya bei ya mazao ya kilimo sokoni kwa wauzaji, wanunuzi na wafanyabiashara.

HUDUMA 4 SEHEMU MOJA

Faida Nyingi

- Inalenga kutatua changamoto za upatikanaji wa taarifa za ugani nchini.
- Kuongeza ufanisi na ufahamu juu ya mbinu bora za kilimo endelevu.
- Kupunguza gharama na muda wa kutafuta huduma za ugani na taarifa.
- Kuhamasisha shughuli za kilimo, mifugo na uvuvi.
- Kuongeza usalama wa chakula na lishe.
- Kuboresha maisha hasa vijijini.

INAPATIKANA KUPITIA SIMU JANJA, SIMU YA KAWAIDA, TABLETS, APLIKESHENI YA ANDROID NA KOMPUTA KUPITIA WAVUTI

- Pakua aplikesheni ya Ugani Kiganjani kupitia Android PlayStore.
- Tembelea tovuti ya <https://digital.apps.fao.org/home>
- Au piga *152*00# kupokea taarifa kupitia ujumbe mfupi wa simu kwa kujisajili kupitia M-Kilimo.

Skani hapa kupakua Aplikesheni.



© Unsplash/Andis Mansoor/Unsplash



© Dale Johnson/500px.com



© Niels Smit/500px.com